***Tuma maoni yako kuhusu Taasisi yetu ikiwemo Mitaala na mambo mengine yanayohusu Taasisi ya Elimu juu ya uboreshaji wa huduma zetu kupitia barua pepe inayotumika kukusanya maoni maoni@zie.go.tz***



**Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya elimu Zanzibar ndugu Abdalla M Mussa akiwa katika picha ya pamoja na ugeni kutoka Wizara ya elimu ya Ethiopia uliongozwa na Mkuu wa Taasisi ya ukuzaji Mitaala ya Ethiopia Bwana Mulukei Nigatu pamoja na maafisa kutoka Shirika la kimataifa ( UNICEF).**

Taasisi ya Elimu ya Zanzibar imekutana na kufanya mazungumzo na Ugeni kutoka Wizara ya Elimu ya Ethiopia uliongozwa na Mkuu wa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Ethiopia Bwana Mulukei Nigatu ambao wameambatana na maafisa kutoka Shirika la kimataifa la kusaidia watoto (UNICEF )Ethiopia pamoja na wakuu wa Idara mbalimbali kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania Kwa lengo la kubadilishana uzoefu wa njia Bora ya uimarishaji wa mitaala.

Kikao hicho ambacho kilifanyika katika ukumbi wa Wizara ya Elimu Mazizini kilikuwa chini ya Mwenyekiti wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Elimu ya Zanzibar Nd Abdalla Mohamed Mussa ambae alimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ,kilijadili hatua mbalimbali ambazo Zanzibar wamezipitia pamoja na faida na changamoto ambazo zimejitokeza wakati wa upitiaji wa Mitaala Zanzibar.





Aidha ugeni ulipata fursa ya kujifunza jinsi ya kuingiza masuala mtambuka katika Mitaala ambapo pia walitembelea kituo Cha Kutoa Elimu (KEMEC )na kituo Cha ubunifu katika Elimu (HUB), mbali na mambo mengine ulitembelea Skuli ya msingi ya Abdala Sheria kwa lengo la kujionea namna ya utekelezaji wa mtaala kwa njia ya ushirikishwaji wa Watoto unavyoleta Tija katika ujifunzaji.

Kwa upande wake mjumbe kutoka Ethiopia amesema ziara hiyo itawasaidia kufikia malengo ya upitiaji wa mitaala Ambapo Kwa nchi yao wanatarajia kufanya mapitio ya mtaala kuanzia mwaka 2024.



**Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya elimu ya Zanzibar ndugu Abdallah M. Mussa, akifunga warsha ya kutafsiri miswada ya vitabu vya kiada na viongizi vya mwalimu katika kituo Cha Amali Makunduchi**





# Kupitia Mihutasari na viwango vya kujifunza

**Baadhi ya watendaji wa Taasisi ya Elimu ya Zanzibar pamoja na wadau wengine wa Elimu 20/7/2023 wameanza kazi ya kupitia Mihutasari na viwango vya kujifunza kuanzia Maandalizi hadi Darasa la saba.kwa skuli za serikali na binafsi ambazo hazifundishi Kwa lugha ya kiengereza.kazi inayofanyika katika kituo Cha mafunzo ya walimu kiembe samaki na kuongozwa na mkuu wa divisheni ya Maandalizi na Msingi kutoka Taasisi ya Elimu ya Zanzibar bi Patima Kheir koba.**



# Kazi ya kutathmini Miongozo



Taasisi ya elimu ya Zanzibar kwa kushirikiana na madrasa early childhood tarehe 11/7/2023 ilianza kazi ya kutathmini miongozo minne ya kufundishia Elimu mjumuisho ambayo ni muongozo wa uchunguzi na utambuzi wa Mahitaji ya kujifunzia,kukuza ujifunzaji mahiri darasani,kuimarisha ushiriki wa wanafunzi na Kuandaa mpango binafsi wa kujifunza na zana za kufundishia huko katika ukumbi wa Elimu mbadala Rahaleo .



Taasisi ya elimu ya Zanzibar Imefanya ziara maalum ya kujifunza mifumo ya Maktaba mtandao jinsi inavyotumika, faida pamoja na gharama za uendeshaji wa mifumo ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa kuanzisha Maktaba ya Taasisi ya elimu zanzibar.hata hivyo uongozi huo wa Taasisi walitembelea ofisi za shule direct kwa lengo la kujionea na kujifunza Maktaba mtandao jinsi inavyo tumika

Kuimarisha Elimu Bora
Improving Quality Education

Kuhusu Taasisi

Taasisi ya Elimu ya Zanzibar ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar iliyoanzishwa mwaka 2011 kwa kuzingatia matakwa ya Sera ya Elimu ya mwaka 2006. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeona kuna umuhimu wa kuwa na chombo cha kuratibu na kusimamia mitaala na utafiti wa elimu ili kuimarisha ubora wa elimu hapa Zanzibar. Kwa mujibu wa Sheria Namba 4 ya mwaka 2016 iliyoanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, Taasisi ina mamlaka ya kutayarisha mitaala, vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa skuli za Maandalizi, Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Elimu isiyorasmi na Watu wazima. Aidha Taasisi inajukumu la kufanya tafiti za kielimu na kutoa mafunzo juu ya utekelezaji wa mitaala.